

UJUMBE MUHIMU KWENDA KWA WATANZANIA.

{KUBADILI WAJUMBE KUWA WATU WAZURI KUPITIA UCHAGUZI WA CCM 2022 NA 2027}

Kama ambavyo Yohana aliyaandikia Mekanisa saba {Ufunuo 1; 9-14} akiwa katika kisiwa cha Patmo, vivyo hivyo nami ninawaandikia Watanzania hasa WanaCCM na wote wenye nia njema na Tanzania nikiwa huku Himaya ya SEKE alikozikwa ***Igulu Bugomola MWANAMALUNDI*** {1840-1936}.

Mwaka 2019 kupitia uchaguzi wa serikali za mitaa CCM ilifanikiwa kupata idadi kubwa ya wenyeviti wa vitongoji, vijiji na mitaa kwa mara ya kwanza tangu mfumo wa vyama vingi uanze. Hata hivyo uchaguzi huo ulikosolewa na wadau wa demokrasia kwa madai ya kuwa wizara yenye dhamana (OR – TAMISEMI) ilivuruga uchaguzi huo kwa kutowapitisha wagombea wengi wa upinzani kwa vigezo mbalimbali ikiwemo kukosea majina yao pamoja na vyama vyao na kufanya wagombea wa CCM wapite bila kupingwa. Kwa hiyo mwaka 2019 kiasi kikubwa cha wapiga kura wa Tanzania hawakutumiza haki zao za kuchagua viongozi wa vijiji na mitaa wanaowataka kutokana na sera zao hadi kupelekea maamuzi ya wajumbe wa vikao vya CCM vilivyopitisha wagombea hao kuwa maamuzi ya mwisho. Kitendo hiki kiliacha sintofahamu kwa wapiga kura wengi wa Tanzania.

Mwaka 2020 vijana na wanawake wengi walijitokeza kushiriki kura za maoni ndani ya chama na kuambulia kura **0,1,2,3,4,5,6,7,8,9** hadi **10** licha ya kujieleza vizuri mbele ya wajumbe kitendo ambacho kilipelekea ‘WAJUMBE SIO WATU WAZURI’ kushika hatamu. Wajumbe wa vikao vya CCM walijipatia jina hilo kwa sababu baadhi yao waligubikwa na vitendo vya rushwa ambavyo viliwapofusha macho na kuchagua kina cha ***mifuko*** ya wagombea na siyo yaliyomo kwenye ***agenda za wagombea***.

Kwa kutambua hilo mwenyekiti wa chama Taifa na rais wakati huo hayati Magufuli aliongoza chama kufanya maamuzi magumu ya kutowapitisha wagombea walioongoza kura za maoni kwenye baadhi ya majimbo kama hatua ya haraka ya kupambana na rushwa pamoja na ‘***UMAFIA***’ mwingine ambao chama kiliona haukubaliki kuhalalisha ushindi huo. Inawezekana CCM chini ya Magufuli ilikuwa na nia njema ya kupambana na rushwa lakini kitendo cha kutowapitisha washindi wa kura za maoni kwenye baadhi ya majimbo kiliacha ***chuki moyoni*** na ***furaha usoni*** kwa baadhi ya wagombea, wajumbe na wapiga kura.

Hata hivo uchaguzi mkuu 2020 ambao chama chetu kilifanikiwa kupata idadi kubwa ya Madiwani na Wabunge ulikosolewa sana na wadau wa demokrasia pamoja na umoja wa mataifa kupitia shirika la haki za binadamu kwamba uchaguzi haukuwa wa huru na haki kwasababu ya maandalizi mabovu ya tume ya Taifa ya uchaguzi ya wakati huo.

Nimeona tujikumbushe hayo kabla hatujaingia kwenye uchaguzi wa chama na kutoa mapendekezo yangu juu ya nini kifanyike ili tupate ‘***WAJUMBE WAZURI***’ kupitia uchaguzi wa CCM 2022 ambao utatupatia wajumbe watakaopiga kura ya maoni kuchagua wagombea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa 2024 na kupiga kura ya maoni kuelekea uchaguzi mkuu wa Madiwani, Wabunge na Rais 2025.

NINI KIFANYIKE?

1. KUWASHILIKISHA VIONGOZI WA DINI, KUENDELEA KUWAKUMBUSHA WAUMINI (WANA CCM) JUU YA UMUHIMU WAO KUJITOKEZA KUGOMBEA NAFASI ZA UONGOZI NDANI YA CHAMA 2022

‘*umkabidhi BWANA njia yako pia umtumaini naye atafanya*’ Zab:37:5

Ni vizuri kutambua nguvu ya imani zetu hasa tunapopambana na rushwa kwa vitendo maandiko matakatifu yanatueleza kuwa rushwa ni adui wa haki lakini pia Mtume Mohammed amesema mtoa rushwa na mpokea rushwa wote motoni

Barack Obama alisema *'I am a big believer in the separation of church and the state but not the separation of religion and Politics. I reject the ideology that sees religion has a purely private activity that must be kept away from Politics'*

Tafsiri isiyo rasmi ni kwamba *" mimi ni muumini mkubwa wa kutenganisha Kanisa na Nchi lakini siyo kutenganisha Dini na siasa. Ninakataa dhana inayoona Dini ina shughuli binafsi ambayo inatakiwa kutenganishwa na mfumo wa maisha yetu,siasa.*

Kwahiyo si dhambi kuwakumbusha waumini wenzetu kwenye madhehebu yao kuzidisha mapambano dhidi ya rushwa kwa vitendo kwa **kugombea** nafasi za uongozi kwenye vyama vyao hasa wana CCM ambao wanatarajia kufanya uchaguzi wa chama 2022 ili kupata wajumbe wenye **hofu ya Mungu** ambao watapiga kura za maoni 2024 na 2025 kwenye uchaguzi wa Madiwani, Wabunge na Rais. Kama tutashindwa kutumia mda huu kabla ya mwaka 2022 kuhamasisha wanachama ambao wanakataa rushwa kugombea nafasi hizo tutajikuta tunarudia makosa ya nyuma ya kuacha vita vya mfukoni iamue nani awe kiongozi wetu 2025 na tutalazimika kusubiri uchaguzi wa chama tena **2027**.

Kukabidhi vita hii kwa Mungu siyo unyonge, ni muhimu sana kwani hakuna jamii iliyoendelea kwa kuongozwa na viongozi ambao ni zao la rushwa. Kuendelea kulalamika kwamba wajumbe si watu wazuri ni ishara mbaya ya kukiri kuwa hatuna uwezo wa kubadili kinachoendelea kwenye chama chetu. Tuchukue hatua muda ni sasa. Christmas na Mwaka mpya havipaswi kupita bila kuyazungumza haya Msikitini, Madhabahuni na Altareni kama tuna nia ya kubadili kinachoendelea.

2. CHAMA CHA MAPINDUZI KINATAKIWA KUANDAA BAJETI YA UANDAAJI NA USIMAMIZI WA UCHAGUZI WA VIONGOZI WAKE KIKAMILIFU.

'Arrogance makes an Easy target'' CRAIG CRAWFORD

Kupitia uchaguzi wa mwaka 2020 ndani ya chama nilifanya utafiti nikagundua kuwa baadhi ya wana chama wa CCM wamekuwa wakitumia gharama kubwa **kufadhiri** uchaguzi kwa njia za panya ili kuhakikisha nafasi za uongozi za chama zinachukuliwa na watu ambao wanatabia za kuuza kura zao kwa kiasi kadhaa cha pesa kwa wagombea pindi muda wa kura za maoni unapofika, vitendo hivyo vichafu vinafanyika kwa njia zifuatazo;

- a. Kuwachukulia fomu na kuwawezesha fedha ili washinde nafasi ya uongozi wa chama kwaajili ya kuwatumia miaka ya uchaguzi wa serikali unapofika (2024, 2025)**
- b. Kutoa usafiri na chakula muda wa uchaguzi jambo ambalo lilipaswa kufanywa na chama**

Chama chetu kinapaswa kujiandaa kikamilifu ili kutowapa mwanya wafadhiri (Sponsors) wa uchaguzi ndani ya chama kwa kujizatiti katika maswala ya maandalizi ya uchaguzi.

CCM ina vyanzo vingi vya mapato hivyo inaweza kuchukua sehemu ya hazina yake ili **kuihami demokrasia ndani ya chama** na kuwafanya wajumbe kuwa huru dhidi ya watia nia wanao jiandaa mfukoni . P.L.O Lumumba aliwahi kusema *'Commercialization of politics is a threats to democracy'* kwa tafasiri isiyo rasimi ni kuwa **kuirasimisha siasa kuwa biashara ni hatari kwa demokrasia**

3. USIMAMIZI WA UCHAGUZI WA CCM 2022 UFANYIKE KWA MFUMO WA OPERATION

'usijisifu kwaajili ya kesho ; kwamaana hujui yatakayozaliwa na siku moja''Mithali 27:1

Hakuna ubaya wa kuiga jambo zuri. Mfano viongozi na maafisa wa chama wanagawana majukumu ya kwenda kwenye majimbo na wilaya kuongeza nguvu ya usimamizi wa uchaguzi kwenye eneo moja hadi jingine. Viongozi na maafisa wa chama waliotumwa na chama waandae **taarifa maalum** ya uchaguzi juu ya namna walivyofanikiwa kudhibiti vitendo vya rushwa kwenye maeneo waliyoaminiwa kutekeleza wajibu huo na kuikabidhi kwa chama. Taarifa hiyo itakisaidia chama kufanya tathmini juu ya vita dhidi ya rushwa ili chama kijue kimefanikiwa wapi na kimeshindwa wapi ili kuongeza ufanisi wa wajumbe kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa 2024 na uchaguzi mkuu 2025 katika kuchagua Diwani, Mbunge na Rais

4. KUANDAA MATANGAZO YENYE LENGU LA KUWAELIMISHA WANACHAMA KUELEKEA UCHAGUZI 2022 NA KUTUMIA VYOMBO VYA HABARI NA MITANDAO YA KIJAMII KUFIKISHA UJUMBE ULIOKUSUDIWA.

Kutokana na uwepo wa vyombo vya habari kama TBC,ITV,STARTV,channel 10,Uhuru FM,magazeti na mitandao ya kijamii inaweza kuelimisha wanachama wetu kabla muda wa uchaguzi haujafika. Kwa mfano maoni kama haya yakipewa fursa kwenye vyombo vya habari vya chama na visivyo vya chama nafikiri kwamba kunachochote kinaweza kupatikana kwa lengo la kuboresha hali yetu kwa sasa

MWISHO


Kupitia barua ya pongezi niliyopokea kutoka chama cha mapinduzi wilaya ya Kakonko/Buyungu yenye **Kumb. No CCM/KNK/U.2/VOL.3/168 ya tarehe 8/11/2020** ilinisisitiza kutokata tamaa ndani ya chama na kuendelea kukijenga na kukiimarisha mahali popote kwa maslahi mapana ya chama na serikali yake kwa kuendelea kushauri na kushirikisha kwa nia ya kukiimarisha chama chetu kiendeleo kuwa madhubuti.

Haya ni maoni yangu ambayo nimeona niwashirikishe ili kuboresha na hatimaye tupate wajumbe 2022 ambao watakuwa na kazi ya kuongoza chama kama viongozi na kupiga kura ya maoni katika uchaguzi wa serikali za mitaa 2024 na **uchaguzi mkuu 2025**.

Kujiandaa vizuri kutafanya CCM kuwa na wajumbe ambao watachagua wagombea wanaonadika kwenye kampeni katika chaguzi za serikali za mitaa 2024 na uchaguzi mkuu 2025 na kupunguza lawama za wapinzani wetu juu ya matumizi ya nguvu ya vyombo vya dola.

Hakuna ulazima wa kuchukua ushauri huu maana tangu mwanzo nimesema haya ni maoni yangu kwahiyo nishukumiwe kwa lolote.

**KIDUMU CHAMA CHA MAPINDUZI
MUNGU AWABARIKI**



ELIA MICHAEL KANJERO
0623525758/0747707312

Nakala: Katibu wa CCM Wilaya-Kwa taarifa

S.L.P 5

KAKONKO.

Katibu wa CCM Mkoa,

S.L.P 199

KIGOMA